Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.21 - 2022

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaendelea kuboresha Elimu yetu*




# Tanzania na Afrika Kusini zatia saini Hati ya Makubaliano ushirikiano maeneo mbalimbali ElimuMsingi



**- KAZI IENDELEE -**




**BODI YA UHARIRI**

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Pongezi Tanzania, Afrika Kusini kusaini Hati ya Makubaliano ushirikiano ElimuMsingi

Julai 7, 2022 Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilisaini Hati ya Makubaliano (MoU) baina yake na Serikali ya Jamhuri ya Afrika Kusini kupitia Idara ya Elimu Msingi ya nchi hiyo ili kuanzisha mashirikiano katika eneo la elimu msingi.

Kusainiwa kwa Hati hiyo ya Makubaliano kutawezesha nchi hizi mbili kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya elimu msingi ikiwemo kubadilishana wataalamu wa kufundisha na kujifunza lugha ya Kiswahili.

Tukio hilo kushuhudiwa na Mhe. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanyika Siku ya Kiswahili Duniani ni katika kuendelea kuipa heshima na kuthamini lugha yetu kama urithi wetu.

Pia ni hatua kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania katika kuendelea kuikuza lugha ya Kiswahili katika mataifa mengine ikikumbukwa kuwa ni lugha ya kwanza ya Kiafrika kutambuliwa kimataifa na UNESCO.

Taasisi za ElimuMsingi zinapaswa kuwa tayari kuhakikisha utekelezaji wa Hati hiyo ya Makubaliano unafanyika vizuri ili lugha ya Kiswahili iweze kueleweka nchini Afrika Kusini na kuamsha morali kwa mataifa mengine kupenda kutumia lugha ya Kiswahili.

Hongera Mhe. Profesa Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Mhe. Matsie Angelina Motshekga Waziri wa ElimuMsingi Afrika Kusini kwa kufungua fursa ya kukiendeleza Kiswahili katika nchi ya Afrika Kusini.



Maelekezo >

# Mkenda: Simamieni miradi ya ujenzi kwa weledi wa hali ya juu

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) amezitaka taasisi zinazotoa taaluma kuhakikisha zinasimamia kwa weledi utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya ujenzi katika taasisi za Serikali.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mjini Unguja, Zanzibar katika kikao na Viongozi na watumishi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati akikagua majengo ambayo ujenzi wake ulisimama kwa muda mrefu, Prof. Mkenda amesema Wizara haitavumilia taasisi yoyote iliyo chini yake ambayo inafundisha wataalamu inashindwa kusimamia kazi inayopewa kwa weledi na kusababisha hasara kwa Serikali.

Waziri huyo ameongeza kuwa anataka kuona taasisi zote ambazo zina jukumu la kuandaa wataalamu katika maeneo ya ujuzi na taaluma mbalimbali zikisimamia kazi zinazopewa kwa ubora na kwa viwango vinavyotarajiwa.

Ameongeza kuwa Serikali inaamini Vyuo na Taasisi za mafunzo vina uwezo wa kusimamia miradi mbalimbali kwa kuwa wana wataalamu ambao wanaandaa wanafunzi vizuri hivyo hazitashindwa kutekeleza miradi kwa weledi kutokana na utaalamu walio nao na kwamba hawatashindwa kuwaondoa viongozi wa taasisi hizo ambao watashindwa kusimamia kwa weledi.

"Taasisi zinazopewa jukumu la kusimamia miradi ya Serikali na hasa Mradi huu wa "HEET" ni lazima kuwa na weledi kuhakikisha kazi zinafanyika kwa wakati na kwa ubora, sina wasiwasi kuhusu utaalamu najua wataalamu wapo tena tunawajua kwa majina lakini kazi wanazozisimamia zikikosa ubora, hatutasita kuchukua hatua. Fedha za mradi huu ni mkopo hata kama riba yake ni ndogo bado Watanzania wataulipa," amesisitiza Waziri Mkenda.

Ameongeza kuwa watu wengi wamekuwa wanataka kuona nchi inakwenda kwenye elimu ujuzi na Vyuo Vikuu vinatoa elimu taaluma, jambo ambalo kama nchi haiwezi kuacha kwani bado inataka kuona watu wanafanya tafiti za kutatua changamoto za nchi, lakini fedha za Mradi wa HEET zenyewe zimeelekezwa zaidi kwenye kujenga ujuzi na ndio maana zimepelekwa kwenye taasisi zinazojenga ujuzi ikiwemo hii ya Sayansi za Bahari Zanzibar ambayo inatoa mafunzo yanayojenga ujuzi katika nyanja mbalimbali za Uchumi wa Buluu.

Mbunge wa Jimbo la Kiembesamaki Mhe. Mohamed Maulid amemhakikishia Waziri wa Elimu kuwa katika nafasi yake ya uwakilishi na usimamizi wa taasisi hiyo watahakikisha inatoa elimu kwa vitendo ili kuwapatia wanafunzi wake ujuzi unaostahili huku akiiomba Serikali kuona namna ambavyo inaweza kuipatia meli ya mafunzo ambapo kwa sasa wanaendelea na utaratibu wa kutumia ngalawa pamoja na meli za kukodi.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) Mosses Mbiru amesema pamoja na ufinyu wa miundombinu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimeendelea kutatua changamoto hiyo kwa hatua mbalimbali ambapo Serikali ya Zanzibar ilitoa eneo la Buyu na Serikali ya Muungano ilitoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia, kutayarisha mchoro, kupata mkandarasi pamoja na kuanza ujenzi katika eneo lenye ekari 123.

Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo imepewa majukumu ya kufanya tafiti katika nyanja zote za Sayansi ya Bahari, kutoa mafunzo ya Uzamili na Uzamivu katika sayansi za bahari, kutoa mafunzo ya Shahada ya Awali kulingana na mahitaji ya Taifa ya wataalamu pamoja na kushiriki katika juhudi za matumizi endelevu ya maliasili za bahari kwa kutoa taaluma kwa nadharia na vitendo.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) unaofadhiliwa na Banki ya Dunia ambao unalenga kuleta nageuzi ya kiuchumi kupitia utoaji wa elimu ya juu kwa kujenga miundombinu, kununua vifaa wezeshi vya kujifunzia na kusomesha Wahadhiri ambapo vyuo vikuu 14 na Taasisi nane za Serikali zitanufaika ikiwemo IMS.



xx

Uimarishaji Sayansi >



xxxx

# Serikali kuimarisha Taasisi ya Sayansi za Bahari kukuza Uchumi wa Bluu

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) imeipatia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam zaidi ya Sh Bilioni 11 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika Taasisi ya Sayansi za Bahari.

Akizungumza mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki mara baada ya kutembelea Taasisi hiyo Mhe. Prof. Adolf Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amesema fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza baadhi ya miundombinu hiyo ambayo ujenzi wake ulisimama kwa muda mrefu.

Ameongeza kuwa fedha hizo zimepelekwa katika Taasisi hiyo ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aligiza fedha zilizopatikana kutokana na Mradi wa HEET kusambazwa nchi nzima ili ziweze kuboresha na kujenga vyuo vitakavyowapatia ujuzi na ajira Watanzania.

"Maelekezo ya Mhe. Rais kuhusu fedha za mradi huu ni kusambazwa kwa nchi nzima ili kuboresha na kujenga miundombinu pamoja na kutoa ajira kwa watu mbalimbali, ndio maana tumeleta fedha hizi hapa lakini pia zimekwenda Tabora, Musoma, Mara, Geita, Simiyu, Manyara, Tanga na kwingineko," amesema Prof Mkenda.

Waziri huyo amekitaka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhakikisha kinasimamia kwa weledi fedha hizo ili zifanye kazi ambayo imekusudiwa kwa ubora na viwango vilivyokubalika.

Aidha, Prof Mkenda amemtaka Makamu Mkuu wa Chuo cha Ardhi, Prof. Evaristo Riwa kufika katika Taasisi hiyo ili kuona mapungufu ya mradi wa ujenzi wa baadhi ya miundombinu iliyojengwa chini ya usimamizi wa chuo hicho na kurekebisha mapungufu hayo kabla ya kuanza kwa awamu nyingine.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki Mhe. Suleiman Haroub amesema fedha hizo zilizotolewa zimeamsha matumaini kwa wananchi wanaozunguka Taasisi hiyo kwani baada ya kuona misingi ya miundombinu hiyo imekaa muda mrefu bila kuendelezwa walijua kinachofuata ni kuondolewa katika eneo hilo na kuahidi kushirikiana na Taasisi hiyo kulinda mazingira na miundombinu.

Mbunge wa Jimbo la Kiembesamaki, Mhe. Mohamed Maulid ameishukuru Wizara ya Elimu na Serikali kwa kutoa fedha za uendelezaji wa ujenzi wa miundombinu na kwamba itakapokamilika itakuwa Taasisi nzuri yenye kuzalisha vijana watakaoshiriki katika kuendeleza uchumi wa bluu.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari, Mosses Mbiru amesema fedha hizo zinakwenda kukamilisha jengo la utawala na taaluma pamoja na kutekeleza azma ya upanuzi wa shughuli za Taasisi hiyo.

Utekelezaji >

# Uzinduzi wa Shule Jumuishi ya mfano ya Sekondari Patandi wafana

Wito umetolewa kwa Viongozi wa taasisi na wadau wanaojishughulisha na utoaji wa Elimu Jumuishi, kuendelea kushirikiana na Serikali katika kujenga shule kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Wito huo umetolewa Jijini Arusha na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga (Mb) wakati akizindua rasmi Shule Jumuishi ya Mfano ya Sekondari Patandi.



xx




xx

Amesema shule hiyo imejengwa na Serikali kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 3.8 na mpaka sasa ina jumla ya wanafunzi 288 wakiwemo 217 wenye mahitaji maalum na 72 wasio na mahitaji maalum.

"Serikali inatambua kuwa pamoja na kuwa na mfumo wa Elimu Jumuishi, bado kuna wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao hawawezi kutumia mfumo huo kutokana na changamoto walizo nazo hivyo ni muhimu kuweka msukumo zaidi katika kuimarisha mifumo tofauti ya ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kama vile shule maalum na vitengo," ameongeza Mhe. Kipanga.

Prof. Carolyne Nombo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu amewashukuru wazazi kwa kuwapeleka watoto wenye mahitaji maalum katika shule hiyo ili kupata Elimu.

"Naendelea kuwatia moyo na kuwapongeza wazazi kutoka sehemu mbalimbali nchini kwa kuwaleta watoto kuja kupata elimu katika shule hii jumuishi ya Patandi," amesema Prof. Nombo.

Naye Dkt. Charles Msonde, Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI amesema Wizara yake imeleta walimu bora na mahiri kuja kufundisha shuleni hapo na ameahidi kuzifanyia kazi changamoto zote ambazo zipo katika shule hiyo ili kuendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji shuleni hapo. "Kazi ya walimu hawa inaonekana wazi ilivyo bora kwa jinsi wanavyowapa watoto hawa maarifa, ujuzi na stadi kwa nadharia na vitendo. Naamini baada ya miaka minne tutashuhudia makubwa sana kutoka kwa watoto hawa," amesema Dkt. Msonde

Akifafanua kuhusu shule hiyo, Dkt. Magreth Matonya, Mkurugenzi wa Elimu Maalum, Wizara ya Elimu amesema shule hiyo sio maalum bali ni jumuishi kwa kuwa inachukua wanafunzi wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji maalum.

"Ukisema shule maalum ina maana inachukua watoto wa aina moja tu yaani wenye mahitaji maalum, lakini shule hii ni jumuishi inachukua na wasio na mahitaji maalum ili wote waweze kusoma kwa pamoja," ameongeza Dkt. Matonya.

Utekelezaji Miradi>

# Kamati ya Kudumu ya Bunge yakoshwa utekelezaji miradi ATC



*xx*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa jengo la madarasa, maabara na ofisi (Ufundi tower) lililopo katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) ambalo ujenzi wake unatekelezwa na fedha za Uviko-19 zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Daniel Sillo alibainisha hayo wakati Kamati hiyo ilipotembelea na kukagua ujenzi wa jengo hilo linalogharimu kiasi cha Sh. bilioni 2.27 ambalo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 90.

Alisema fedha hizo zimesaidia ujenzi wa madarasa nane yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 880 kwa wakati mmoja, maabara sita zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 270 kwa wakati mmoja pamoja na ofisi 26 zenye uwezo wa kuchukua watumishi 104.

"Hapa tumeona jinsi fedha za Uviko-19 zinavyofanya kazi, tunampongeza Rais Samia kwa kuhakikisha Vyuo vya ufundi vinajengwa ili kusaidia jamii kuongeza ujuzi na kuleta tija katika Taifa letu," alisema Mhe. Sillo.

Naye Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omari Kipanga amesema Serikali inaendelea kuboresha vyuo mbalimbali ikiwemo kujenga vyuo vinne vya ufundi katika mikoa ya Rukwa, Geita, Njombe na Simiyu ambapo Shilingi bilioni 20 zimepelekwa kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo. Ameongeza kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa Shilingi milioni 523 kwa ajili ya kununua samani za kutumika katika jengo hilo.

"Tupo katika mchakato wa kuboresha mitaala ya elimu ambayo ikianza kutumika itawezesha wanafunzi kupata elimu yenye ujuzi, ubunifu na kuongeza ajira," ameongeza Mhe. Kipanga.

Naye Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha, Dkt. Musa Chacha alishukuru Serikali kwa kuhakikisha inaongeza tija kwa vyuo vya ufundi huku akieleza kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa na maabara.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa jengo hilo pia kutapunguza msongamano wa wakufunzi katika ofisi sanjari na kuboresha ratiba za masomo ikiwemo kuondoa baadhi ya vipindi kufundishwa muda wa jioni sana na hata nyakati za usiku kutokana na uchache wa madarasa na maabara.

Nao baadhi ya Wabunge wa Kamati hiyo akiwemo Halima Mdee walikipongeza chuo hicho kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 2,017 mwaka 2015/16 hadi kufikia wanafunzi 4,693 mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 100.

Aliongeza kuwa kuna ongezeko la wanafunzi wa kike 769 kutoka waliokuwepo mwaka wa masomo

## Uboreshaji ElimuMsingi >

# Tanzania na Afrika Kusini zatia saini Hati ya Makubaliano ushirikiano maeneo mbalimbali ElimuMsingi



*xxx*

Serikali imesema itaongeza nguvu kazi, miundombinu na bajeti kwa taasisi na vyuo vinavyofundisha kiswahili ili viendelee kuandaa wataalam zaidi watakaotumika Duniani kote.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yanayofanyika jijini Dar es Salaam kwa njia ya simu Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema Serikali itaendelea kutoa nyenzo na mafunzo ya kisasa kwa wakalimani, waandishi wa vitabu, wafundishaji wa Kiswahili kwa wageni.

Katika Maadhimisho hayo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Elimu ya Msingi ya Jamhuri ya Afrika Kusini zimetia saini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika mambo mbalimbali ya Elimu ya Msingi ikiwemo kufundisha kiswahili.

Utiwaji wa saini umefanywa mbele ya Mhe. Philip Isidor Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof Adolf Mkenda kwa upande Tanzania na kwa Jamhuri ya Afrika Kusini umefanywa na Waziri wa Elimu ya Msingi Matsie Angelina Motshekga

Akiongea kabla ya utiaji wa saini Prof. Mkenda amesema baada ya kukamilika kwa maandalizi ya Hati hiyo Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza kutiwa saini rasmi makubaliano hayo siku ya Kiswahili Duniani.

"Kazi ya kuandaa makubaliano haya ilifanyika kwa muda ikiongozwa na viongozi mbalimbali ambapo baada ya kukamilika Rais alituagiza tusaini makubaliano haya leo katika siku hii muhimu kwa nchi yetu," amesema Pro. Mkenda

Naye Matsie Angelina Motshekga, Waziri wa Elimu ya Msingi wa Afrika Kusini amesema lengo la kusaini hati hiyo ni kufundisha Kiswahili katika shule za msingi na vyuo pamoja na kukisambaza nchi nzima ili kuwawezesha waafrika Kusini waweze kuitumia lugha ya Kiswahili.

Motshekga ameongeza kuwa kwa Afrika Kusini Kiswahili ni zaidi ya lugha kwani ni muhimu sana kwani kitasaidia kuunganisha watu wake na Bara la Afrika ambapo Kiswahili kinaongelewa zaidi.

" Kiswahili kwa Afrika Kusini kitaunganisha watu wa Tanzania na kwetu pamoja na kuimarisha mahusiano ya muda mrefu yaliyopo kati ya nchi hizi mbili, na ni lazima tuhakikishe lugha hii inaunganisha watu wetu hususani vijana" ameeleza Waziri huyo wa Afrika Kusini.




*xxx*



xxx

# Benki ya Dunia yatembelea Shule ya Sekondari Turiani

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Kusini mwa Afrika, Bi Victoria Kwakwa Julai 11, 2022 ametembelea shule ya Sekondari Turiani Jijini Dar es Salaam ili kujionea maendeleo ya Programu ya SEQUIP ambayo sehemu ya utekelezaji wake ni mpango wa kuwarudisha shuleni watoto walioacha masomo kutokana na sababu mbalimbali ili waweze kuendelea na masomo yao.

Akizungumza shuleni hapo akiwa ameongozana na mwenyeji wake Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof Adolf Mkenda kiongozi huyo amesema amefurahi kupata nafasi ya kutembelea shule hiyo na kuona mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza sekta ya elimu ili kuzalisha nguvu kazi.

Amepongeza kwa hatua aliyochukuliwa na Mhe. Rais ya kuwapa tena fursa wanafunzi ambao walikatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ili wapate elimu ambayo itawawezesha kujiletea maendeleo kwao wenyewe na familia zao pamoja na kuchangia katika uchumi wa Taifa.

Kwakwa amesema Benki ya Dunia itaendelea kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha watoto wa Kitanzania wanapata elimu bora kwenye miundombinu na mazingira salama ya kujifunzia pamoja na kuondoa changamoto zinazokwamisha mchakato wa ujifunzaji.

Akizungumza katika ziara hiyo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof Adolf Mkenda amesema Serikali ina mkakati mkubwa wa kuhakikisha watoto wote walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito wanarudi na kuendelea na masomo yao.

Kiongozi huyo amesema benki hiyo imefadhili programu ya SEQUIP ambayo imewezesha kuwarudisha shuleni wanafunzi wapatao 3,333 ambao waliacha shule kutokana na sababu mbalimbali ambapo takribani wanafunzi 900 wamerudi katika mfumo rasmi na wengine katika mfumo wa elimu mbadala.

Ameongeza kuwa Makamu wa Rais huyo amefika katika shule hiyo ili kuona na kuongea na mabinti waliorudi shule kupitia programu ya SEQUIP inayofadhiliwa wa Benki ya Dunia ili kuangalia maendeleo yao.



xx

Nidhamu, Weledi kazini >

# Katibu Mkuu Michael ataka watumishi TET kuendelea kufanya kazi kwa nidhamu



xxx



xxx

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt.Francis Michael amewataka watumishi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kufanya kazi kwa weledi, nidhamu katika kuhakikisha suala la elimu linaendelea kuimarika nchini.

Dkt.Michael ameyasema hayo leo tarehe 11/7/2022 jijini Dar es salaam alipofanya ziara katika Taasisi hiyo ambapo amesema Serikali inawategemea katika kusaidia utoaji wa elimu nchini.

"Nawaomba mfanye kazi kwa weledi na kuhakikisha suala la elimu na haswa haya maboresho ya mitaala yanayoendelea yafanyike vizuri,"amesema Dkt.Michael.

Aidha Dkt.Michael amemshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoendelea kuwajali watumishi wa umma kwa kujali maslahi yao na kuwataka watumishi wa TET kutomwangusha Rais, na badala yake wafanye kazi ipasavyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Dkt. Aneth Komba amesema kuwa wameshukuru ujio wa Katibu Mkuu na kuwa TET inaendelea kufanya kazi zake katika kuzingatia misingi ya kiutumishi na kuwa suala la maboresho ya mitaala linaloendelea litafanyika vizuri.

Katibu Mkuu katika ziara yake aliambatana na Mkurugenzi wa Rasilimali watu na Utawala wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Moshi Kabengwe.

## NUKUU >

**SERIKALI INATAMBUA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM NCHINI NA NDIO MAANA INAZIFANYIA KAZI ILI KUWEKA MAZINGIRA WEZESHI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI.**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

**Katibu Mtendaji**
Tume ya Vyuo Vikuu,
S.L.P. 6562, DAR ES SALAAM
es@tcu.go.tz

**Mkurugenzi Mtendaji**
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
S.L.P. 76068, DAR ES SALAAM
adcp@heslb.go.tz / ed@heslb.go.tz

**Katibu Mtendaji**
Baraza la Mitihani la Tanzania, (NECTA)
S.L.P. 2624 au 32019, DAR ES SALAAM
esnecta@necta.go.tz

**Mtendaji Mkuu**
Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, (NACTE)
S.L.P. 7109, DAR ES SALAAM
info@nacte.go.tz

**Mtendaji Mkuu**
Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, (ADEM)
S.L.P. 71, BAGAMOYO
adem@adem.ac.tz

**Mkurugenzi Mkuu**
Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, (COSTECH)
S.L.P. 4302, DAR ES SALAAM
dg@costech.or.tz / info@costech.or.tz

**Mkurugenzi Mkuu**
Taasisi ya Elimu Tanzania, (TET)
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM
director.general@tie.go.tz

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),
S.L.P. 34578, DAR ES SALAAM
info@tea.or.tz na dg@tea.or.tz

**Mkurugenzi Mkuu**
Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA),
S.L.P. 2849, DAR ES SALAAM
info@veta.go.tz / pr@veta.go.tz

**Mtendaji Mkuu**
Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)
S.L.P. 743, ARUSHA
dg@taec.go.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo,**
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),
S.L.P. 35091, DAR ES SALAAM
vc@admin.udsm.ac.tz / relation@admin.udsm.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo,**
Chuo Kikuu Ardhi (ARU),
S.L.P. 35176, DAR ES SALAAM
aru@aru.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), S.L.P. 65001, DAR ES SALAAM
vc@muhas.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA),
S.L.P. 3000, MOROGORO
vc@sua.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu Mzumbe (MU),
S.L.P. 1, MOROGORO
mu@mzumbe.ac.tz / info@mzumbe.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu cha Dodoma,
S.L.P. 259, DODOMA
vc@udom.ac.tz / prelations@udom.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),
S.L.P. 23409, DAR ES SALAAM
vc@out.ac.tz

**Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),
S.L.P. 2329, DAR ES SALAAM
principal@duce.ac.tz / dpacademic@duce.ac.tz

**Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi,
S.L.P. 474, MOSHI
info@mocu.ac.tz

**Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa,
S.L.P. 2513, IRINGA
principal@muce.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),
S.L.P. 131, MBEYA
vc@mustnet.ac.tz

**Makamu Mkuu wa Chuo**
Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 447, ARUSHA
vc@nm-aist.ac.tz

**Makamu Mkuu cha Chuo**
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,
S.L.P. 976, BUTIAMA, MARA
info@mjnuat.ac.tz

**Mkurugenzi**
Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania,
S.L.P. 9283, DAR ES SALAAM
info@tlsb.go.tz

**Katibu Mtendaji**
UNESCO,
S.L.P. 20384 DAR ES SALAAM
info@natcom.go.tz

**Mkurugenzi**
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW),
S.L.P. 20679, DAR ES SALAAM
info@iae.ac.tz

**Mkuu cha Chuo**
Chuo cha Ufundi Arusha,
S.L.P. 296, ARUSHA
rector@atc.ac.tz / pro@atc.ac.tz

**Mkurugenzi,**
Kituo cha Maendeleo Dakawa,
S.L.P. 1733, MOROGORO

**Mkuu wa Chuo**
Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),
S.L.P. 2958, DAR ES SALAAM
principal@dit.ac.tz

**Mkuu wa Chuo**
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193, DAR ES SALAAM
rector@mnma.ac.tz